

**BABA YANGU NISIKIZE**

1. Bismillah nianze, kwa jina lako L'atifu,  
Abu nimuelekeze, njiayo iliyo kufu,  
Naomba asipuuzi, akawa mpuuzifu,  
Ewe babangu Rajabu, hebu uende kuhiji.
2. Siyo kwamba nakuhoji, katu, nakupa mnofu,  
Baba uende kuhiji, wende pata uongofu,  
Uje uwe Al-hajji, wa mapana na marefu,  
Ewe babangu Rajabu, upesi nenda kuhiji.
3. Nitafurahi hakika, baba ukiwa shafu,  
Hasa ukifika Makka, ukaondoe uchafu,  
Hakika utapendeka, mimi Aga nasadifu,  
Ewe babangu Rajabu, hebu uende kuhiji.
4. Ikiwa takabalia, tayarisha masurufu,  
Muda ukishafikia, uushike Msahafu,  
Ndege ukiipandia, uende patakatifu,  
Ewe babangu Rajabu, upesi nenda kuhiji.
5. Haki nakwambia baba, mimi Aga mkosefu,  
Abu nenda Alkaba, na uwe mkumbukifu,  
Fungua yako akiba, isiyo na upungufu,  
Ewe babangu Rajabu, hebu uende kuhiji.
6. Hamidu ninayo hamu, abu uwe mkunjufu,  
Uzivae ihramu, kabula hujatawafu,  
Makka ukasitakimu, Hija iwe kamilifu,  
Ewe babangu Rajabu, upesi nenda kuhiji.
7. Kisamba nenda haraka, Hamidu nakuarifu,  
Alkaba kuzunguka, bila ya kutakalifu,  
Huko akhi ukifika, hakika nitajisifu,  
Ewe babangu Rajabu, hebu uende kuhiji.
8. Ni wangapi wanafika, si vikongwe si vipofu,  
Kwa kuwa njia ya Makka, kwa watu idhihirifu,  
Hivyo ufanye haraka, uzihesabu sarafu,  
Ewe babangu Rajabu, upesi nenda kuhiji.
9. Ni wangapi wanakwenda, wasio hata turufu,  
Wembamba na walokonda, wenye pumzi hafifu,  
Sembuse we ulowanda, rijali ulo nadhifu,  
Ewe babangu Rajabu, hebu uende kuhiji.
10. Baba nenda harakia, uwe insi mtiifu,  
Naona unakawia, nauli ni tahafifu,  
Haya piga totalia, fedha zisije kashifu,  
Ewe babangu Rajabu, upesi nenda, kuhiji.
11. Usijali nauli, hata makumi elfu,  
Ikienda kwa Jalali, ndipo utaposhafu,  
Ondoka toka Katuli, ukamuombe Raufu,  
Ewe babangu Rababu, hebu uende kuhiji.
12. Mimi wazi nakwambia, Aga nina upungufu,  
Mola hajanijalia, nikatambua Alifu,  
Abu ungejionea, naamba si ubunifu,  
Ewe babangu Rajabu, hebu uende kuhiji.
13. Na tena nakuambia, ni kazi ya ukosefu,  
Elimu nilofatia, yenye mengi mapungufu,  
Kuliwaa Qurania, utungo wake L'atifu,  
Ewe babangu Rajabu, hebu uende kuhiji.
14. Yangu mengi sintosema, kwani si ya takalifu,  
Anayajua Rahima, aliye mkamilifu,  
Mimi sasa nayasema, hayo yalo lainifu,  
Ewe babangu Rajabu, upesi nenda kuhiji.
15. Hamidu nitakuwaje, jinsi nitavyojisifu,  
Abu ukienda nje, Makka ukenda halafu,  
Hata kisha yake uje, na hijayo kamilifu,  
Ewe babangu Rajabu, hebu uende kuhiji.
16. Masembe uende kwanza, tumbaku lima halafu,  
Hivi sasa wewe anza, kuandaa masurufu,  
Kila kitu kutimiza, kuepusha usumbufu,  
Ewe babangu Rajabu, upesi nenda kuhiji.
17. Nenda harakia nenda, akhi wangu mtukufu,  
Nataka uje mshinda, aletaye takilifu,  
Huyo Rajimia punda, apendaye waongofu,  
Ewe babangu Rajabu, hebu uende kuhiji.
18. Jibu nalitegemea, jibu lisilo hafifu,  
Jibu la kupendezea, masikio ya L'atifu,  
Jibu lililo zuria, limridhi Mtukufu,  
Ewe babangu Rajabu, upesi nenda kuhiji.
19. Haya baba fikiria, niliyoyapanga safu,  
Haki utanisifia, ikiwa nimesadifu,  
Pia unisamihia, iwapo ni mpunjufu,  
Ewe babangu Rajabu, hebu uende kuhiji.
20. Nimshukuru Jalia, Mola wangu Mtukufu,  
Kwa kituo kufikia, baada kupanga safu,  
Baba yangu kimbilia, Makka kabula tawafu,  
Haya baba harakia, uende Makka kuhiji.

*Hamidu R. Tambwe*